

SWAHILI FORUM 22 (2015): 42-71

MWINGILIANOMATINI KATIKA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

AMBROSE K. NGESA, ENOCK MATUNDURA & JOHN KOBIA

Tamthilia ya Kiswahili imedhihirisha, kwa njia moja au nyingine, uhusiano wa kimwingilianomatini. Makala haya yanadhamiria kuchunguza viwango na aina za mwingilianomatini baina ya tamthilia mbili za Kiswahili. Tamthilia hizi ni *Mashetani* (Hussein 1971) na *Kijiba cha Moyo* (Arege 2009). Tathmini hii inaongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Tumeteua na kuhakiki tamthilia hizi kwa misingi kwamba, kwa muda mrefu, Ebrahim Hussein ameaminika kuwa mmojawapo wa watanzi bora wa tamthilia ya Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki. Wahakiki wa fasihi wanaelekea kukubalia-na kwamba Ebrahim Hussein ameathiri watanzi wengi wa baadaye wa tamthilia kimitindo, kimaudhui na usawiri wahusika. Lengo la makala haya ni kujaribu kuonesha jinsi tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* zinavyofanana kwa kuchunguza viwango vya mwingilianomatini baina ya tamthilia hizo kwa kurejelea, motifu, maudhui, matumizi ya lugha, na wahusika. Je, ni kwa kiwango gani mtunzi wa *Kijiba cha Moyo* ameathiriwa na mtunzi wa *Mashetani*? Je, amemnukuu, kudondoau kumwiga mtangulizi wake kwa kiwango gani?

Utangulizi

Fasihi, kama sanaa nyingine yoyote ile ni chombo chenye misingi yake katika ubunifu. Vilevile tamthilia ni aina ya sanaa inayotumia lugha ili kuendeleza tajiriba za binadamu (Njogu & Chimerah 1999). Fasihi inaweza kuwa simulizi au andishi. Fasihi andishi ina tanzu zake kuu ambazo ni riwaya, hadidhi fupi, ushairi na tamthilia. Tamthilia ni utungo wa kifasihi unaowasilisha hadithi na migongano kwa kutumia maongezi na matendo ya wahusika (Wafula 2003). Mtungo huu unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa lakini wenyewe kuliweka wazo linalotaka kuwasilishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira.

Miongoni mwa watanzi maarufu wa tamthilia mbao wameacha taathira kubwa mno katika utanze huo Afrika ya Mashariki ni Ebrahim Hussein¹. Athari zake kwa watanzi chipukizi zinadhihirika kwa namna mbalimbali. Lengo la makala haya ni kutathmini jinsi athari za kazi mojawapo ya Ebrahim Hussein, *Mashetani* (1971) inaingiliana kimatini (mwingilianomatini)² inapolinganishwa na kazi ya mtuzi wa baadaye, *Kijiba cha Moyo* (Arege 2009). Kipindi kinachotenganisha utunzi wa kazi hizi mbili ni takriban miongo minne. Lengo la makala haya ni kujaribu kuonesha namna tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* zinavyofanana kwa

¹ Ricard (2000) kwa mfano anadai kwamba Ebrahim Hussein “ni mtunzi bora zaidi wa tamthilia ya Kiswahili.”

² Hii ni dhana ya kifasihi inayohuishwa na mnadharia wa Kifaransa, Julia Kristeva ambaye aliiuzua kutokana na nadharia ya Mikhail Bakhtin ya Usemezano. Dhana hii hutumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi za kifasihi. Kama nadharia ya kifasihi, mwingilianomatini huchukulia kwamba kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine. Makala haya yanajaribu kuonesha jinsi tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* zimeingiliana na kuhusiana katika kile kinachowenza kuitwa ‘mwanda wa kimwingiliano-matini.’

kuchunguza viwango vya mwingilomatini baina ya kazi hizi kwa kurejelea, motifu³, maudhui, matumizi ya lugha, na watusika. Je, ni kwa kiwango gani mtunzi wa *Kijiba cha Moyo* ameathiriwa na mtunzi wa *Mashetani*? Je, amemnukuu, kudondoa au kumwiga mtangulizi wake, na kwa kiwango gani?

Historia fupi ya Tamthilia ya Kiswahili

Tamthilia ya Kiswahili ilianza kuwekwa katika hali ya maandishi kuanzia miaka ya 1950. Tamthilia za kwanza kabisa zilitokana na michezo ya kuigiza iliyohusishwa na wazungu waliofika Afrika Mashariki. Tamthilia hizi zilishughulikia maudhui sahili ya ucheshi ambayo yalilenga kuwafurahisha watazamaji. Kwa sababu hii, watunzi wa wakati huu walitumia mtindo sahili kuwasilisha maudhui yao. Graham Hyslop aliyeanza kazi ya uigizaji 1944 alikuwa mgeni wa kwanza kuhusishwa na michezo hii ya kuigiza. Mwaka wa 1957, aliandika michezo miwili ya kuigiza: *Afadhal Mchawi* na *Mgeni Karibu*. Baadaye, watunzi wenyeji wa Afrika Mashariki kama vile Henry Kuria na Gerishon Ngugi walianza kutunga tamthilia. Mnamo 1953, Kuria aliyekuwa mwanafunzi wa Hyslop, alitunga tamthilia ya *Nakupenda Lakini...* iliyochapishwa mwaka wa 1957.

Mbali na tamthilia zilizotungwa kwa Kiswahili, kuna zile ambazo zilitafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, zilizochangia sana katika ukuzaji wa utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Baadhi ya zile zilizotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili (*Makbeth* (Mushi 1968), *Tufani* (Mushi 1969), *Julius Kaizari* (Nyerere 1969), na *Mabepari wa Venisi* (Nyerere 1969) mionganoni mwa nyingine. Hata hivyo utanzu wa tamthilia ya Kiswahili uliendelea kuimarika kiufundi na kimaudhui baada ya uhuru kutokana na michango ya watunzi wengi wa Afrika Mashariki (Wafula 1999; Ntarangwi 2004).

Baada ya uhuru, watunzi wa Kiafrika walijitoma katika ulingo wa utunzi wa tamthilia na zenye maudhui ya uovu na udhalimu wa wakoloni. Waandishi hawa walijitosa uwanjani kuousha mwamko wa Waafrika katika kupigania ukombozi, huku wakionyesha kila dhuluma na uonevu waliofanyiwa na wakoloni. Baadhi ya watunzi wa kipindi hicho ni pamoja na Ebrahim Hussein katika *Kinjeketile* (1969) na Mugyabuso Mulokozi katika *Mukwawa wa Uhehe* (1979)⁴ (Ntarangwi 2004). Baadaye kulizuka utambuzi mionganoni mwa waandishi asilia wa Kiafrika

³ Dhana hii hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya kifasihi. Huweza pia kutumiwa kuelezea elementi fulani ya kimaundu na kimaudhui inayotawala kazi fulani. Kwa mfano, katika riwaya za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) Kezilahabi ametumia motifu ya safari ambapo mhusika mkuu ('mimi') yuko safarini kuusaka ukweli. Tazama pia riwaya ya *Siku Njema* (1996) ya Walibora ambapo mhusika mkuu anafunga safari kutoka Tanzania kwa minajili ya kumsaka baba yake mzazi nchini Kenya.

⁴ *Mukwawa wa Uhehe* (Mulokozi 1979) ni mojawapo ya tamthilia ya Kiswahili iliyotumia kiunzi cha juhudi za mashujaa wa Kiafrika katika ukombozi wa jamii zao kutokana na dhuluma za wakoloni. Tamthilia nyingine katika pote hili ni *Kinjeketile* (Hussein 1969).

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

waliogundua kwamba kuondoka kwa mkoloni hakukusitisha kamwe dhuluma ya ukoloni, kwani ukoloni mkongwe uliacha nyuma kimelea cha ukoloni-mamboleo. Kwa sababu hii, tamthilia za *Mashetani* (Hussein 1971) na *Kilio cha Haki* (Mazrui 1982) zilitungwa kuangazia maudhui ya ukoloni-mamboleo, unyanyasaji wake, mifumo ya kisiasa na sera za jamii katika nchi zilizo-jipatia uhuru wa kisiasa (Wafula 1999).

Kuanzia miaka ya 1990 hadi wa sasa, utunzi wa tamthilia ya Kiswahili umeonekana kuimarika kiufundi na kimaudhui. Hata hivyo tukichunguza kwa makini tamthilia hizi kwa njia moja au nyingine, zinarejelea sana tamthilia zilizozitangulia hasa zile zilizoanza kuukemea uongozi mbaya wa Waafrika baada ya kujinyakulia uhuru pamoja na kuonyesha athari zilizoachwa nyuma na mkoloni (Wafula 1999). Uhusiano huu huathiri usomekaji wa matini mpya kwa kuiruhusu matini tangulizi iiathiri kwa kiwango fulani (Enani 1995). Ni katika ngazi hii ambapo makala haya yamedhamiria kuonesha na kubainisha uhusiano huu katika *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*.

Dhana ya Mwingilianomatini

Dhana ya mwingilianomatini inarejelea msingi kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo huhusiana na matini nyingine na miundo ya lugha yenyewe. Dhana hii husisitiza kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambapo hujibizana; kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa (Plotell & Charney 1978). Aidha, matini zote huhusiana kwa njia moja au nyingine, na vilevile matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia ya mwingilianomatini ni pamoja na:

- i. Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi.
- ii. Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbali mbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.
- iii. Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja, ambapo matini tangulizi hufyonzwa na kujibiwa na matini mpya.
- iv. Matini za kifasihi huwa zimechota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine.
- v. Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi huigeuza kwa kiwango. Kwa jinsi hii kauli inayonukuliwa hubadili na kuelezea upya kauli asilia kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kisisimu na kijamii.

Suala la mwingilianomatini limechunguzwa na wasomi kadha, hasa kuhusiana na utanzu wa riwaya⁵ (Bodunde 1994, Kehinde 2003, Rohde 2005, Diegner 2005, Njoroge 2007, Walibora

⁵ Baadhi ya riwaya za Kiswahili zinazoingiliana katika kiwango cha uhusika, msuko na mandhari ni *Maumbile si Huja* ya (Habwe 1995) na *Asali Chungu* ya (Mohamed 1978). Tazama pia kazi zifuatizo: *Sitaki Iwe Siri*

2011 na Nwagbara 2011). Wataalamu hawa wamedhihirisha kuwa, matini za kifasihi huhusiana kwa njia moja au nyingine, jambo ambalo huifanya kila matini kuwa ni mwingiliano (Kristeva 1966, 1981, 1986, Culler 1975, Barthes 1979, Allen 2000, Diegner 2005 na Njoroge 2007). Hivyo basi kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, uhusiano wa kimwingiliano baina ya matini hupatikana katika tanzu zote kuu za fasihi. Ingawa uhusiano huu hupatikana katika tanzu zote za fasihi, utanzu wa riwaya umehakikiwa sana kwa kutumia mkabala wa nadharia ya mwingilianomatini huku tanzu nyingine kama vile tamthilia zikikosa kushughulikiwa sana.

Tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* zimeteuliwa kimakusudi kwa sababu zilitungwa katika vipindi tofauti vya kihistoria. Tamthilia ya *Mashetani* ilichapishwa mnamo mwaka wa 1971 huku *Kijiba cha Moyo* ikichapishwa 2009. Ingawa masafa ya muda baina ya kuchapishwa kwa kazi hizi ni takriban miongo minne, tahakiki ya jicho kali inabainisha kwamba kazi hizi zinafanana kwa kiwango fulani. Vilevile kwa mujibu wa Wafula (1999), tamthilia ya *Mashetani* iliweka tarehe mpya katika utungaji wa mchezo wa kuigiza katika lugha ya Kiswahili. Tamthilia hii ilionyesha, kwa mafanikio makubwa, jinsi mapokeo ya Kiafrika yanavyoweza kutumika pamoja na mbinu za kisasa kufanikisha malengo ya kijukwaa. Aidha kwa muda mrefu Hussein amekuwa mtunzi mashuhuri wa tamthilia tata za Kiswahili aliyezea kuathiri watunzi wa baadaye si kimtindo na kimaudhui tu, bali pia jinsi huwasawiri wahusika, na pia urejelezi wake wa mazingira ili kuyaelezea maudhui yake (Ricard 2000). Hussein alitunga tamthilia ya kihistoria ya *Mashetani* (1971) iliyotatanisha wahakiki na watunzi wengi. Katika karne ya ishirini na moja, Arege naye amekwisha kutunga tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) akifuata mtindo wa kuitunzi uliotumiwa na Hussein *Mashetani*. Hali hii inatuchocha kujaribu kuchunguza na kubainisha mfanano wa kimaudhui, kimtindo na usawiri wa wahusika baina ya tamthilia hizi mbili.

Kumhusu mwandishi Ebrahim Hussein

Ebrahim Hussein alizaliwa Kisiwani Kilwa mnamo 1943, alikokulia na kusomea. Katika ujana wake, Hussein alikuwa mwanaharakati wa chama cha kisiasa cha Tanzania African National Union (TANU). Baadaye aliacha kuwa mwanaharakati wa siasa za taifa lake baada ya kukosa imani na siasa. Hussein alianza kutunga michezo ya kuigiza mwishoni mwa miaka ya sitini. Kama mwandishi, aliendelea kusomea masuala ya kazi za drama. Aliwahi kwenda Ujerumani kwa masomo ya juu kuhusu drama katika miaka ya sitini (Bertонcini *et al* 2009). Kama mzawa wa Uswahlini, Hussein alibuni na kuzalisha sanaa zake kutokana na mazingira na tamaduni za Uswahlini.

(Matundura 2008) na *Nataka Iwe Siri* (Kirumbi 1974), *Usiku Utakapokwisha* (Msokile 1993) na *Giza Limeingia* (Mbogo 1980). Riwaya fupi ya Msokile ya *Usiku Utakapokwisha* kwa mfano inasimulia hadithi ile ile inayopatikana katika tamthilia ya Mbogo ya *Giza Limeingia*. Tofauti ya pekee ni ya utanzu na majina tu. Badala ya Kopa na Mashaka katika *Giza Limeingia*, kuna Gonza na Chioko katika *Usiku Utakapokwisha*.

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Mbali na *Mashetani* (1971), tamthilia zake nyingine ni pamoja na *Wakati Ukuta* (1967), *Alikiona* (1967), *Kinjeketile* (1969), *Jogoo Kijijini* (1976), *Ngao ya Jadi* (1976), *Arusi* (1980) na *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988). Tamthilia za Ebrahim Hussein zinasomwa sana katika shule za upili, vyuo vya walimu na vyuo vikuu nchini Kenya.

Kumhusu mwandishi Timothy Arege

Timothy Arege ni mzaliwa wa Kaunti ya Kisii magharibi mwa Kenya. Alisomea kuko huko kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi, ambapo alijipatia shahada ya B.A. (Kiswahili na Sayansi ya Kijamii). Mnamo mwaka wa 1998 alipata shahada ya Uzamili (MA) katika taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Mnamo 2013, alipata shahada ya Uzamifu katika chuo hicho hicho. Mwaka wa 2008/2009, Arege alituzwa kuwa msomi bora na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki⁶, Kenya. Vilevile mwaka wa 2011, Arege alishinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta⁷ mnamo 2009 kwa kazi yake Kijiba cha Moyo (2009). Kwa sasa Arege ni mhadhiri wa somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Tamthilia zake nyingine ni pamoja na *Chamchela* (2007) na *Mstahiki Meya* (2009).

Muhtasari wa Tamthilia ya Mashetani

Tamthilia ya *Mashetani* ni ya nne ya Hussein. Illichapishwa mwaka wa 1971. Kazi hii ni mojawapo wa tamthilia za Kiswahili zinazofungamana na majilio ya ukoloni, pamoja na kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni katika maeneo ya Afrika Mashariki. Tamthilia hii inaangazia ukengeushi wa wasomi wa Kiafrika, jinsi mkoloni aliyyouporomosha utamaduni wa Kiafrika, na hatimaye kuonesha ‘kinyang’anyiro’ cha kuidhibiti miundomsingi iliyoachwa na mkoloni. Aidha inaonesha jinsi watawaliwa walivyoziinduka na kuanza kupigania uhuru wao, pamoja na kujikita kwenye masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini Tanzania na Afrika kwa jumla (Wafula 2003). Ilitungwa wakati jamii nyingi za Afrika Mashariki zilikuwa zinakumbwa na mabadiliko makuu ya kisiasa, kijamii na kiuchumi (Matundura 2012). Katika kipindi hicho, jamii za Kiafrika zilikuwa zinakumbana na athari za utamaduni wa kimagharibi uliorutubishwa na elimu na dini ya kigeni. Mgogoro uliopo baina ya Shetani (Juma) na Binadamu (Kitaru) katika kijitamthilia wanachokiigiza wahusika hawa unapambanua kile kinachowakilishwa na lile gari la ‘benz’ ya

⁶ Awali, Timothy Arege alikuwa mhadhiri wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kitakoliki cha Afrika Mashariki, Nairobi Kenya kabla ya kuhamia katika Chuo Kikuu cha Kenyatta ambako anahudumu kwa sasa.

⁷ Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta (sasa ikijulikana kama Text Book Centre Jomo Kenyatta Literature Prize) ambayo hutolewa na Chama cha Wachapishaji cha Kenya mara moja baada ya miaka miwili ndiyo tuzo maarufu ya fasihi nchini Kenya na Afrika Mashariki na Kati. Tuzo hii hutolewa kwa waandishi bora wa fasihi wanaotunga kwa Kiswahili na Kiingereza nchini Kenya katika tanzu zote kuu za fasihi ikiwemo fasihi ya watoto. Tuzo ya kwanza ilitolewa mnamo 1974, lakini kwa sababu ya misukosuko ya ukosefu wa hela, haikuweza kuendelea kutolewa. Ilifufuliwa mnamo 1992 baada ya kupata udhamini kutoka Text Book Centre. Mwandishi Timothy Arege ndiye wa kwanza kuishinda tuzo hiyo mnamo 2011 katika utanze wa tamthilia baada ya kutunga *Kijiba cha Moyo*.

babake Kitaru katika tamthilia kuu. Mgogoro huu ndio mwangwi wa kuzitazama hulka za baadhi ya wahusika wa tamthilia kuu kama vile; Bibiye Juma kutamani maisha ya ubwana wa kibwanyenye kama ilivyokuwa zamani bali na kulia ngoa kila wakati; Mfaume kuchorwa akiamini kwamba mashetani wapo.

Katika *Mashetani*, Hussein amezieleza athari za mkoloni kwa kutumia jazanda⁸ kama vile Shetani na Binadamu, chewa na mkondo, jahazi na abiria pamoja na pango. Amezilinganisha athari hizi na zile azipatazo mtu aliyepagawa na pepo au mashetani. Hussein anatoa kauli kuwa sharti njia za kuzipunga athari hizi zitafutwe ili Mwfrika aweze kuwa huru.

Muhtasari wa Kijiba cha Moyo

Kijiba cha Moyo ni tamthilia iliyotungwa na Arege na kuchapishwa 2009. Ni mojawapo ya tamthilia tatizo zilizowahi kuandikwa katika fasihi ya Kiswahili. Tamthilia hii ina mtindo changamano. Ina sehemu sita, na kila sehemu ina maonyesho yake na wahusika ambao kila mmoja anaigiza nafasi yake. Tamthilia hii inawasilisha matukio na visa ambavyo ama vinaibuka au vinashawishi uhusiano baina ya mataifa yaliyostawi na yale yanayoendelea. Mwandishi ame-mchora mhusika mkuu katika tamthilia hii akiwa mwenye maumivu lakini anayekana maumivu yake. Mhusika huyu ni mwenye kujisaili yeye mwenyewe na pia anaisaili jamii yake. Anataka ajue nafasi yake katika jamii, na vilevile nafasi ya jamii yake katika ulimwengu, unaomilikiwa na nguvu za kibepari. Mambo yanayomsumbu ni ishara ya yale yanayoisumbua jamii pana ya taifa lake, na jamii ya Kiafrika kwa ujumla.

Tamthilia hii inaangazia uhusiano uliopo baina ya mataifa yanayoendelea (mataifa machanga), hasa ya Kiafrika na yale yaliyoendelea (madola makuu). Uhusiano huu unaelezwa kuwa wa mnyonge na mwenye nguvu. Katika uhusiano huu, mnyonge hunyanyaswa na kudhulumiwa na mwenye nguvu kila wakati. Mataifa makuu duniani huendeleza utawala mpya wa kiuchumi uliozuka baada ya wakoloni kuondoka barani Afrika. Mataifa haya huendeleza mfumo wa kibepari wa kikapitalisti kupitia kwa utoaji wa ufadhili, ruzuku na katika utekelezaji wa miradi yao. Wakati kuna amani duniani, mataifa makuu huzua michafuko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ili mataifa machanga yayakimbilie kwa usaidizi ambao hutolewa kupitia ufadhili, ruzuku, misaada na pia uwezekaji. Kwa njia hii mataifa makuu huyafanya mataifa machanga kuendelea kuyategemea.

⁸ Istilahi hii kimsingi inahusiana na taswira. Hata hivyo, hutumiwa kuelezea hasa sifa za matumizi ya picha au taswira kwa ujumla wake. Tunaposema kwamba kazi fulani ina jazanda, tunalenga kwenye ujumla wa matumizi ya taswira ambazo zinaweza kuwa za aina mbalimbali (Syambo na Mazrui 1992: xvi).

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Mwingilianomatini wa Kimaudhui katika Mashetani na Kijiba cha Moyo

Mwingilianomatini tulivyotaja awali huchunguza jinsi matini hurejeleana, kuathiriana, kutoa mwangwi⁹ na pia jinsi matini maalumu hurudia maudhui na miktadha ya matini tangulizi na kuibadili ili kutekeleza jukumu la mtunzi (Culler 1981, Bloom 1994, Mishra 2012). Aidha, mwingilanimatini ni dhana inayorejelea mkabala wa usomaji na uandishi wa matini kama njia mojawepo ya kuchunguza jinsi matini maalumu huingiliana na matini zilizoitangulia, waandishi, wasomaji wa awali, pamoja na makubaliano yake.

Dhana hii hutumika sana katika utafiti wa fasihi linganishi ambaeo huzingatia desturi zinazoangazia mlinganisho, mlinganuo na mwathiriano baina ya waandishi na vilevile baina ya matini. Desturi ya fasihi linganishi na maendeleo ya kifasihi hurejelewa kwa dhana ambazo hudhihirisha jinsi sanaa ya mwandishi fulani hufyonzwa na kuingizwa katika muktadha wa utamaduni mwingine.

Kwa mujibu wa Njogu & Wafula (2007), wataalamu wanaouna mawazo ya nadharia ya mwingilianomatini humtaja Mikhail M. Bakhtin aliyeokuwa mwanaisimu na mhakiki wa kazi za fasihi kuwa wa kwanza kushughulikia uhusiano baina ya matini moja na nyingine hata kabla ya Kristeva kuasi dhana ya mwingilanimatini. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa Bakhtin (1981) alishikilia kuwa kazi ya kifasihi huwa na sauti mbalimbali zinazoingiliana na kutoa mwangwi wa kazi nyingine zilizoitangulia, zilizopo, au zitakazokuja baadaye. Kimsingi kazi ya kifasihi ya kimwingilianomatini huwa na uwezo wa kuhusiana, kuingiliana na kurejeleana na kazi nyingine za kifasihi kwa njia tofauti tofauti.

Mwingilianomatini katika Maudhui ya ukoloni Mamboleo

Ukoloni mamboleo ni namna utawala wa nchi za kibepari huathiri na kuamua kuhusu uchumi na siasa za nchi zinazoendelea kwa maslahi yao. Kwa namna hii mataifa makuu huendelea kuyadhibiti mataifa ya madogo kwa njia zisizo za moja kwa moja. Waandishi wa tamthilia hizi mibili wanaonesha kwamba mataifa ya Kiafrika yangali yanadhibitiwa na mataifa ya Kimagharibi kiuchumi na kisiasi. Waandishi hawa wanayarejelea matukio ambayo yanadhihirisha kuwa mataifa ya Kiafrika yamekosa uhuru wa masuala muhimu ya kiuchumi na kisiasi. Kwa hivyo mataifa hayo yalipewa uhuru wa bendera. Mataifa yaliyo na uwezo huendelea kuathiri matukio ya kisiasi pamoja na kumiliki nyezo kuu za uzalishaji mali katika mataifa ‘huru’ ya Kiafrika.

⁹ Kauli ya mwangwi hapa inatumika kumaanisha kwamba matini moja ya kifasihi inamrejesha msomaji katika matini nyingine aliyotangulia kuisoma na labda kumsaidia kuilewa kwa urahisi matini anayoisoma kwa sasa. Kwa mfano *Utenzi wa Hati* ni utungo aliotunga Shaaban Robert kama wosia kwa binti yake. Tazama *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1966). Mwangwi wa utungo huu unatolewa kwenye *Utendi wa Mwana Kupona* (1858) ultiitungwa na Mwana Kupona binti Mshamu kama wosia kwa binti yake. Kimuundo tungo hizi zinakaribiana, maudhui yake yanakaribiana ingawa hapa na pale Shaaban Robert anajaribu kuyapinga baadhi ya mawazo yapatikanayo katika utenzi huo.

AMBROSE K. NGESA, ENOCK MATUNDURA & JOHN KOBIA

Kulingana na King'ei (1987), wakoloni walijitayarishia tabaka la wenyeji lililokuwa na mwelekeo sawa na wao kupitia elimu na dini kabla ya kutoa uhuru. Tabaka hili lilitumiwa na wakoloni kulinda na kudumisha maslahi yao katika mataifa ‘huru’ ya Kiafrika. Mataifa yaliyorejelewa katika tamthilia za *Mashetani* na Kijiba cha Moyo yalijikuta katika hali hii baada ya kipindi fulani cha kupewa ‘uhuru’ wao.

Hata hivyo, ukoloni mamboleo hudhihirishwa pia na mgawanyiko wa matabaka ya kijamii. Aghalabu matabaka hayo huwa ya kibwanyenye na kinaizi. Katika tamthilia ya *Mashetani*, familia ya Juma na familia ya Kitaru ni viwakilishi vya matabaka haya mawili makuu ya kijamii. Familia ya Juma inawakilisha tabaka la “kibwanyenye” lililokuwa la matajiri wa kiukoo. Tabaka hili lilimiliki mali nyingi ilioirithiwa kutoka kwa wavyele wao. Tabaka la “kinaizi” linaashiriwa na familia ya Kitaru. Tabaka hili lilikuwa la watu waliopokea elimu ya Kizungu na ndilo lililosika hatamu za uongozi katika serikali iliyoundwa baada ya mapinduzi ya 1964. Baadaye lilikuja kujulikana kama tabaka la wazungu weusi na lilirithi vyeo, nyumba na mienendo ya kimaisha iliyoachwa nyuma na wakoloni.

Lakini wengi katika wao, chambacho Mwalimu Nyerere, walikuwa Wazungu weusi.
(Utangulizi wa *Mashetani*: vii)

Kadhalika, ukoloni mamboleo hudhihirishwa na kuwepo kwa unyanyasaji na dhuluma kwa mnyonge. Hali hii ya unyanyasaji na dhuluma inadhihirika katika tamthilia hizi mbili ingawa kila mwandishi anaichora hali hii kivyake. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mashetani*, Hussein anaiendeleza hali hii akitumia senema ya *Cowboy* (mwenye nguvu) na Red Indians (mnyonge). Kwa upande mwingine Arege anaiendeleza hali hii katika Kijiba cha Moyo akitumia mfano wa papa (mwenye nguvu) na vidagaa (wanyonge). Hili lashadidiwa na vifungu vifuatavyo:

JUMA; Twende senema basi. Itakusaidia.

KITARU: Hakuna senema nzuri.

JUMA: Iko cowboy moja. Tikiti juu yangu.

KITARU: Senema yenye nina jua hata kabla sijaiona. **Cowboy** atawaua **Red Indians** wote peke yake. Mimi mchezo unaonyesha ugomvi au mgongano baina ya mwenye nguvu na asiye na nguvu, siupendi.

(Mcheko unaongezeka.)

JUMA: Alaa.

KITARU: Tena isitoshe kila siku yule yule tu **anaonewa**. Hakuna hata siku moja ambayo **anaonea**. **Anaonewa** yeeye tu. (*Mashetani*: 18, msisitizo wetu)

ZAINABU: Shangazi, Sele ana tabia za ajabu sana siku hizi kama nilivyokueleza. Anasema eti **anawaonea vidagaa** huruma kuliwa na **papa** na yeeye awale. (Kimya.) Anasema huku ni **kuonewa** mara dufu. Anasema ... eti tena hapendi **vinavyoliwa** huku vinatazama tu. (*Kijiba cha Moyo*: 15-16, msisitizo wetu)

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Senema za *Cowboy* zilikuwa zikitumiwa na wakoloni miaka ya sitini kuonyesha uwezo na nguvu zao dhidi ya Waafrika. Katika miaka elfu mbili, kulizuka kauli mbalimbali zilizolenga kuonyesha uwezo na nguvu za tabaka tawala. Mojawapo ya kauli hizi ilikuwa ni ‘samaki wakubwa’ (papa), wakihusishwa na ‘samaki wadogo’ (vidagaa). Ikichukuliwa kuwa waandishi hawa waliandika kazi zao baada ya vipindi hivi (*Mashetani* 1971, *Kijiba cha Moyo* 2009), basi ‘Cowboy’ na ‘Papa’ ni viwakilishi vya mwenye nguvu (mkoloni) huku ‘*Red Indians*’ na ‘vidagaa’ vikiwa ni viwakilishi vya wanyonge. Kwa hivyo vifungu vilivyodondolewa hapo juu vinashadidia kuwa waandishi wa tamthilia hizi mbili wanairejelea hali ya uonevu iliyo sawa. Vifungu hivi vinaonyesha uhusiano uliopo baina ya mataifa machanga ya Kiafrika na madola makuu duniani ambapo mataifa machanga huonewa kila wakati na mataifa wafadhili. wa wanyonge na wenye nguvu kwa kutumia dhana zilizotofauti lakini zinazorejeleana na kukamilishana. Jinsi *Red Indians* wanavyonyanyaswa na kudhulumiwa na *Cowboy* mmoja ndivyo vidagaa wanavyonyonyaswa na kudhulumiwa na papa kwa kuliwa kila wakati.

Waandishi hawa wanaonyesha kuwa hali ya utegemezi ni athari iliyoachwa nyuma na ukoloni mkongwe na hivyo basi kubainika kama kipengele kinachodhihirisha ukoloni-mamboleo. Aidha, hali hii ilitokana na kuwepo kwa ukoloni mpya wa kiuchumi uliyoyakumba mataifa ya Kiafrika. Ukoloni huu uliyafungamanisha mataifa machanga na mataifa makuu kiuchumi na kisiasa (Maidi 2008). Hali hii inaelezewa na mtunzi wa *Mashetani* kwa kutumia mfano wa jahazi naye mtunzi wa *Kijiba cha Moyo* ametumia dhana ya dau. Jazanda wanazozitumia zinalenga kuonyehsa jinsi ambavyo viongozi wa Kiafrika huwategemea wakoloni kwa maongozi yao. Kwa mfano:

KITARU: [...] toka tumepata uhuru, sisi Waafrika imekuwa kama tumeingia ...ehe [...] Katika **jahazi** moja zuri sana na jina letu limeandikwa. Lakini ... **nahodha** ... **nahodha** nani? [...] Ehe, je mkondo ukiwa unavutia upande mwagine, na Nahodha anataka kupeleka jahazi upande mwagine? [...] Ule **mkondo** unatoka ... Katika kinywa cha **shetani** (*Mashetani*: 21, msisitizo wetu)

ZAINABU: Pamoja na hayo, sisi vilevile ni **washika dau**. Ingefaa kutushirikisha mapema.

MUSA: Wajua katika **dau**, kuna **wenye kulishika** na **wenye kushikwa na dau**. Na wakati mwagine tofauti si dhahiri. Kwa ujumla huchukuliwa kuwa wote wanaoliabiria **dau ni washika dau** mpaka pale anapotokea mtu na kueleza kuwa **wenye dau** wapo na wamelitia mkononi. (*Kijiba cha Moyo*: 24-25, msisitizo wetu)

Kutokana na dondo hizi, inadhihirika kuwa viongozi wa mataifa huru ya Kiafrika wanashurutishwa kufuata maagizo ya wakoloni ili kuyaongoza mataifa yao kama asemavyo Sele “... wamepewa amri na ndugu zetu washirika kupitia mikopo yao. Si habari ya sisi kuchangua. Ni sisi tutii.” (*Kijiba cha Moyo*: 29). Ingawa mataifa ya Kiafrika yana majina yao yaliyoandikwa, wao wenyewe siyo manahodha (viongozi), bali wakoloni ndio huendeleza maongozi ya matifa hayo

wakiwa mbali. Mataifa hayo hudhibitiwa na nguvu za wakoloni (mkondo na wenyewe dau) wakiwa mbali. Nguvu hizi za kibepari huyasukuma mataifa huru kufuata mfumo fulani wa kiuchumi au wa kisiasa watake wasitake. Mifano hii ni jazanda pevu zinazoangazia utata unaowakumba viongozi wa mataifa huru ya Kiafrika katika utoaji wa maongozi yao kutokana na kuwepo kwa nguvu za kikoloni zinazoathiri mifumo yao ya kisiasa na kiuchumi.

Watunzi wa tamthilia hizi mbili wametumia hadithi kuhusu viumbe wa baharini kukuza na kuendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo. Mtunzi wa *Mashetani*, ametumia hadithi ya chewa anayesemekana kuwa akivuta pumzi huyaathiri maji yote na kusababisha yaingie kinywani mwake. Aidha huvuta na kumeza mashua yoyote anayoitaka hata kama haitaki. Mtunzi wa *Kijiba cha Moyo* anatoa mwangwi wa hadithi hii akitumia papa na vidagaa katika maisha yao ya baharini. Wanaeleza:

KITARU: Hadithi ya **chewa**. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna **chewa mkubwa**. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa [...] Anaweza kutoka huko aliko, **kuivuta na kuimeza mashua** yoyote [...] Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali shetani. (*Mashetani*: 28, msisitizo wetu)

SELE: Na hapa wapo watu ambao watakuambia kuwa bila pumzi hizo za papa, **vidagaa** vitakufa kwa kukosa hewa ya kuvuta. **Si ajabu basi papa kuvifanya vidagaa kitoweo**. Unaona? (*Kijiba cha Moyo*: 37, msisitizo wetu)

Chewa na papa katika muktadha huu ni viumbe vyenye uwezo katika maisha ya baharini. Kulungana na utafiti huu, ni taashira zinazoonyesha uwezo na nguvu za mfumo wa kibepari unaoendelezwa na wakoloni mamboleo. Aidha ni viashiria vya madola makuu duniani, yanayoendeleza mifumo ya kibepari. Mashua na vidagaa ni viashiria vya mataifa huru ya Kiafrika. Vilevile ni taashira ya wasio na nguvu. Katika tamthilia zote mbili, bahari inasimamia uwanja wa kiuchumi na kisiasa. Maji ni mkondo wa biashara ulimwenguni.

Kwa hivyo katika dondoo zilizonukuliwa, watunzi wa *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* wamefanua kikamilifu maudhui ya ukoloni mamboleo wakitumia mifano tofauti, lakini inayohusiana na kuingiliana. Jazanda hizi zinaonyesha kuwa mataifa ya Kiafrika yanapojiingiza katika mahusiano na mataifa makuu duniani, hukosa uhuru wao kwa maana huanza kuongozwa na nguvu za mataifa hayo makuu.

Mwingilianomatini katika Maudhui ya Elimu ya Kigeni

Tamthilia hizi mbili zinarejelea maudhui ya elimu kwa kuonyesha jinsi elimu ya kigeni ilivyotumika kumgeuza Mwfrika awe kikaragosi wa mkoloni. Halikadhalika, zinadhahirisha jinsi elimu hii ilivyoumbua utu na ujamaa wa Kiafrika na badala yake ikaumba kasumba ya kikoloni akilini mwa Waafrika. Kasumba hii ilienezwa kuitia elimu ya kizungu iliyowafanya Waafrika waache kujithamini na badala yake kujiona kama viumbe duni mbele ya mkoloni. Kwa sababu hii,

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Mwafrika akaanza kujiona akiwa kiumbe duni mbele ya mkoloni, kama inavyodhihirika katika dondoo zifuatazo:

KITARU: [...] Ninajua umeudhika, lakini kwa nini, nikiwa na wewe, ninaona kuwa kuna kitu? Kuna kitu fulani ulichonacho ambacho kinanitenga mimi na **kinanifanya mimi kuwa kama mdogo mbele yako?** Siyo unanidharau, **lakini unanifanya kama mjinga.** (*Mashetani*: 51, msisitizo wetu)

SELE: Sasa nimeona... Mimi na nyinyi na utaalamu wenu. Usayansi fulani. **Lakini zaidi najiona mimi au kitu kama mimi.** Naona nimebanwa na kitu mfano wa kamba...kama gundi vile... kama... niliyekufa ganzi. (*Kijiba cha Moyo*: 73-74, msisitizo wetu)

Tamthilia hizi mbili zinafanana kuhusu jinsi ambavyo zinasawiri athari za elimu ya kimagharibi mionganini mwa mwenyeji (Mwafrika). Kwa mfano, Arege anatumia taashira ya ‘kovu’ na vilevile taashira ya ‘uso’. Taashira sawa na hii ilitumiwa na mtunzi wa tamthilia ya *Mashetani* kama ‘alamu’ na ‘nafsi’ ya shetani. Taashira hizi zinaonyesha jinsi Mwafrika alivyoathiriwa na ugeni akawa hawezi kuithamini vilivyo vyake. Kwa mfano kauli zifuatazo zinashadidia hili:

SELE: Ni kama nilivyokuambia. **Sipendi hili kovu.** Uso kwa jumla. Vyote hivi vinausumbua moyo wangu. Lakini watu wanafikiri kuwa ni kuachishwa kwangu kazi kunakonisumbua... Mimi ninajielewa tofauti na wanavyonielewa. Lakini langu ni hili moja! Sipendi mkao wa uso wangu. Ninauchukia. Unanikera. Sipendi pua hii...Pua mbaya hii... (*Kijiba cha Moyo*: 33-34, msisitizo wetu)

KITARU: [...] Huoni, lakini, kama leo **kila kitendo kina alama ya shetani na kila mtu ana nafsi ya shetani.** (*Mashetani*: 25, msisitizo wetu)

Hata hivyo watunzi wa tamthilia hizi wanakubaliana kuwa athari za mkoloni zinamsumbu Mwafrika kiasi cha kumfanya asijithamini wala kukubali kuwa ni mtu sawa na alivyo mkoloni. Wanakubaliana kuwa kasumba hii ndiyo tatizo linalomsumbu Mwafrika (Kitaru na Sele). Kwa hivyo tamthilia hizi mbili zinadhihirisha mwingilianimatini wa jinsi zinavyowasilisha maudhui ya elimu na athari zake.

Mwingilianomatini katika Suala la Ugonjwa na Matibabu

Maudhui ya ugonjwa na matibabu yameshughulikiwa na waandishi wa tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*. Katika tamthilia hizi, wahusika wakuu wamesawiriwa wakisumbuliwa na ugonjwa usioelewaka. Ugonjwa huu unahuhushishwa na ama mashetani au pepo. Aidha unakusudiwa kuangazia shida zinazoisumbua jamii za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*. Ugonjwa wa Kitaru katika *Mashetani* unatokana na mifumo ya kibepari inayoifunga jamii yake na unashabihiana na wa Sele katika *Kijiba cha Moyo*. Kwa hivyo wahusika hawa wamechorwa wakiwa wanasumbuliwa na fikra nzito ambazo zinawatatiza wanaowaona. Kadhalika, wahusika wakuu katika tamthilia hizi mbili wanaonyesha hisia zilizo sawa wanapozinduliwa kutoka kwa

AMBROSE K. NGESA, ENOCK MATUNDURA & JOHN KOBIA

mawazo yao. Hisia za Sele anapoitwa na Aisha katika *Kijiba cha Moyo* ni sawa na za Kitaru anapoitwa na Mama yake katika tamthilia ya *Mashetani*. Kwa mfano:

(**Anamwona Kitaru yumo fikirani.**) (*Mashetani*: 24, msisitizo wetu)

Nyumbani kwa Kitaru **Kitaru anafikiri** yuko peke yake. Muda mama yake anaingia.

MAMA: Kitaru. (Kimya)

KITARU: (**Anashtuka.**) **Naam.**

MAMA: Mbona umeshika tama baba?

KITARU: **Hata.** Hapana kitu.

BABA: **Unaumwa?**

KITARU: **Hata.** (*Mashetani*: 27, msisitizo wetu)

Hali hii inamfanya mwandishi aeleze kuwa:

Nyumbani. Ukumbini... Sele ameshika tama. **Anaonekana mwenye mawazo mengi.**

AISHA: Sele! (Kimya. Kwa sauti zaidi.) Sele!

SELE: (**Anashtuka.**) **Naam!**

AISHA: (Kwa mshangao.) Una nini Sele? **Unaumwa?**

SELE: **Hata!** (*Kijiba cha Moyo*: 1, msisitizo wetu)

Ugonjwa wa Kitaru ni wa kiistiani kwani yuko mbioni kujaribu kuelewa ubepari uliopo katika jamii yake. Aidha, anataka kujua ukweli uliosababisha tofauti za kiuchumi, kijamii na kisiasa baina ya tabaka la kinaizi na lile la kibwanyenye. Kwa hivyo ugonjwa wa Kitaru ni fikira alizonazo kuhusu vile anavyoweza kutoka katika hali hii ya ukabaila na kisha aweze kujenga uhusiano ulio na maana. Anaeleza kuwa:

KITARU: Nilikuwa nafikiri tu. [...] **Nilikuwa nikifikiria hadithi.**

MAMA: Hadithi! Hadithi gani?

KITARU: Hadithi ya chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba kuna chewa mkubwa [...] **Anaweza kutoka huko aliko na kuivuta na kuimeza mashua yoyote** anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake. Na **huyu chewa siyo chewa bali shetani.** (*Mashetani*: 27-28, msisitizo wetu)

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ugonjwa wa Sele unafanua mgongano wa nafsi zake mbili zinazokinzana. Yeye anajua kwamba kuna kasoro fulani katika jamii anamoishi iliyosababishwa na kuweko kwa nguvu za kikoloni. Nguvu hizo huamua mkondo wa kisiasa na kiuchumi katika taifa lao lililo ‘huru’. Isitoshe, anaelewa kuwa mataifa ya kibepari huonea na kunyanyasa mataifa machanga kwa kuingilia njia za uzalishaji na ugavi wa mali ya mataifa yao. Ugonjwa wake hivyo

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

basi unaashiria matatizo yanayokumba mataifa machanga ya Kiafrika yanayo sababishwa na kuweko kwa ukoloni mamboleo. Anatoa maelezo yafuatayo:

SELE: Sikiliza bibi, hivi ninavyokaa hapa nyumbani si kwamba nimekata tama. La hasha! **Ninajaribu kutafakari kwa makini uhusiano baina yao na sisi.** Navilevile kudadisi sisi ni kina nani katika uhusiano huo. (*Kijiba cha Moyo*: 28-29, msisitizo wetu)

Kila wahusika hawa wanavyoliwazia tatizo la ubepari katika jamii zao ndivyo wanavyozidi kuumia akili. Kwa hivyo mafikra ya kina kuhusu tatizo hili ndiyo yanayowauma. Ugonjwa sawa na huu umeshughulikiwa na Chacha Nyaigotti Chacha katika tamthilia ya *Marejeo* (1986). Kwa hivyo kulingana na vifungu vilivyodondolewa, inabainika kuwa tamthilia hizi mbili zinashabihiana katika ukuzaji na uendelezaji wa motifu ya ugonjwa.

Wahusika wakuu katika tamthilia hizi mbili wanapotambua kuwa kuna kasoro fulani katika jamii zao, wajilingiza kwenye harakati za kujisaka wajijue wao ni kina nani katika mahusiano baina ya jamii zao na jamii za wakoloni. Kujijua huku ni kuielewa historia ya jamii zao, maana ya uhuru wao pamoja na umuhimu wa azimio lao la ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa. Ukweli kuhusu historia na hali ya jamii zao katika siku za mbeleni ungepatikana tu kutokana na kujijua huku. Ni kwa sababu hii raia (*Kitaru na Sele*) wanaamua kusafiri safari ndefu ya kujisaka na kujijua wao ni kina nani katika ulimwengu unaomilikiwa na mfumo wa kibepari. Wanasema:

KITARU: [...] **Lazima njue ukweli ingawa pengine utanumiza.** (Kimya.) Na nitajuaue ukweli? Ukweli ni lazima utafutwe. **Lazima nisafiri, safari ndefu,** nikajitafute, nikajisake ili njijue mimi nani? Ili njue maana ya kitendo chake. (Anaondoka.) (*Mashetani*: 12, msisitizo wetu).

SELE: ... Mimi nahisi kama sisi tunayumbishwa mithili ya miti msimu wa kipupwe. Na **hili limenifanya kuvuta fikra na kuangalia uhusiano wetu sisi na wao, na sisi kwa sisi.** Basi. (*Kijiba cha Moyo*: 29-30, msisitizo wetu).

Ikichukulia kuwa Kitaru na Sele ni viwakilishi vya Waafrika basi wahusika hawa wote wanasumbuliwa na azma ya kutaka kujua chanzo cha mahusiano yasiyokuwa na usawa na haki kati ya mataifa ya Kiafrika na madola makuu duniani. Kadhalika wanatafuta uhusiano ulio jengwa kwenye misingi ya kiutu.

Wanapoanza kutafuta suluhu ya shida zao, kila mmoja wao anaanza kujifungia chumbani mwake. Kwa mfano, Kitaru anajifungia chumbani akipekuapekua vitabu vya historia ili ajue asili ya uhusiano usiokuwa na usawa na haki. Kwa upande mwingine Sele anaanza kukaa chumbani kwake akiwaza kuhusu uhusiano usiokuwa na utu baina ya madola makuu na mataifa ya Kiafrika. Tunajulishwa kuwa:

MAMA: ... **Kila saa mtoto yuko chumbani.** Sijui anafanya nini huko chumbani peke yake.

JUMA: ... Nasikia **unajifungiafungia ndani.** Nini tena?

KITARU: Ah kuna kitabu, hivi ninasoma. (*Mashetani*: 14-15, msisitizo wetu)

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* onyesho la iv, mwandishi anatoa maelezo yafuatayo:

(Siku hiyo hiyo. Magharibi. **Nyumbani kwake Sele. Sele yuko peke yake ...** Anaonekana mwenye mawazo lakini mtulivu.) (*Kijiba cha Moyo*: 27, msisitizo wetu)

Ingawa Arege katika *Kijiba cha Moyo* hatumii maneno yale yale ya Hussein katika *Mashetani*, ameyageuza maneno hayo ili kuwasilisha dhana ile ile ya kujifungia chumbani. Aidha wanakaa peke yao na hivyo basi kuoneka wakiwa hawajielewi wenyewe. Hali hii inawafanya waitiwe madaktari wa kigeni ili waje kuwatibu.

KITARU: [...] Nikawa naijuliza na kufikiri. Wazee wangu **wakamwita daktari.** Naye daktari ana manyoya kama sisi; ke mengi zaidi. [...] (*Mashetani*: 49, msisitizo wetu)

AMRI: ... **Si nyinyi mloanza kumwonyesha hao madaktari?** Sasa anafahamu wapo. Hata ahisi kuwa lipo jambo dogo linalomsumba atakimbia pale pale mlivyo-mwonesha nyinyi. Umleavyo atakuwa hivyo. (*Kijiba cha Moyo*: 63, msisitizo wetu)

Katika tamthilia ya *Mashetani*, daktari analetwa kumtibu Kitaru kutokana na fikra zake ‘chafu’. Daktari huyu hatumiwi kama taswira ya wale wanaotumiwa kutibu magonjwa yoyote yale katika jamii. Ametumiwa kama taswira ya wale wanaotibu magonjwa fulani yanayofungamana na mifumo ya uzalishaji mali. Kwa hivyo madaktari hawa wa kigeni wanaitwa kuja kumtibu nguli (Kitaru) ili akomeshe mwamko wa kisiasa usiotangamana na mifumo kibepari ya watawala (Wafula 1999). Anaeleza:

Ugonjwa huu, ninavyofikiri mimi.... Kwa kweli, pengine ni kuchoka kwa akili tu. Watoto wa chuo kikuu bwana, wana mengi wanayoyasoma na kuyafikiri. Pengine amepata, labda *neurosis*. (uk. 33)

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* daktari anayeletwa kushughulikia matibabu ya ugonjwa wa Sele ni sura ya pili ya mkoloni. Sele anafafanua hivi kwa kuzua fumbo la ‘daktari’ na ‘uso-daktari’ au ‘refa’ na ‘uso-refa’ (uk. 75). Aidha mawazo ya Sele yanaonyesha kuwa wageni (wakoloni mamboleo) husababisha tatizo katika mataifa machanga na wakati ule ule hujitolea kulitatu shida hiyo. Hii ndio maana Sele anaishia kutoa kauli kuwa “Urefa na uso-refa ni pande mbili za sarafu moja” (uk. 75). Daktari huyu anasaidiwa katika shughuli zake na Jamila aliye mwenyeji na aliyesomea taaluma ya udaktari. Ugonjwa wa Sele unaelezwa kwa lugha ya kitaalamu kuwa ni *Body Dysmorphic Disorder*, yaani B.D.D. Unafafanuliwa zaidi kuwa:

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Ni hali ya mtu kujikuta kutoipenda sehemu fulani ya mwili wake na kuichukia. Hutawaliwa na fikra ya ubovu anaoudhania haupo. Muda wake mwangi huwa katika ubovu huo na hufanya kila namna kutaka kuona kuwa hali hiyo imerekebishwa na kuwa anavyotamani iwe... (*Kijiba cha Moyo*: 90-91)

Hussein anamchora daktari anayeushughulikia ugonjwa wa akishindwa kumjibu Kitaru kuhusu kile kinachomsumbu. Haelewi kuwa ugonjwa wa Kitaru unatokana na fikra alizonazo kuhusu hali yao ya kinaizi isiyofungamana na maisha ya kijamaa. Kwa hivyo si maradhi na wala hauko mwilini bali uko akilini mwake. Aidha, Hussein anaonyesha kuwa Daktari, kama vile wazazi wa Kitaru, ni “Shetani” au kabaila na hawezi kutambua tatizo la Kitaru ambalo limetokana na fikira zake juu ya maisha ya kikabaila. Katika ndoto, Kitaru anamwona daktari huyu akiwa ameota manyoya mengi sawa na wazazi wa Kitaru. Kitaru anaeleza kuwa:

KITARU: [...] Nikaanza kujinyonyoa manyoya yangu. Lakini kila nikijinyonyoa, mengine yanaota. [...] makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko yale. [...] Wazee wangu wakamwita daktari. **Naye daktari ana manyoya kama sisi, ke mengi zaidi** [...] Imechukua muda mrefu **kutambua kuwa nilio nikiyaona siyo ndoto au fikira mbovu, bali ni ukweli** wa kawaida. (*Mashetani*: 48-49, msisitizo wetu)

Daktari analetwa ili amtibu Kitaru kutokana na fikra zake za ‘chafu’. Daktari huyu anatumwa kama taswira ya wale wanaotibu magonjwa fulani yanayotangamana na mifumo ya kiuchumi, hasa uzalishaji mali. Yeye alihitajika ‘kumganga’ Kitaru ili asiuonyeshe mwamko wa kisiasa usiotangamana na utashi wa watawala (Wafula 1999).

Kwa upande mwininge, daktari mgeni anayeletwa kumtibu Sele katika *Kijiba cha Moyo* haonyeshi kuelewa wala kujishughulisha kwa kina kulitatu tatizo la Sele. Utaaluma wake unatiliwa shaka na mtunzi wa tamthilia hii. Mtunzi anamfanya daktari wa kigeni ashindwe kuitambua shida ya Sele kwa ili aweze kuonyesha kuwa suluhu ya matatizo ya wenyeji haimo kwa wageni bali kwa wenyeji. Sele anasumbuliwa na fikra alizonazo kuhusu ubepari wa madola makuu duniani, hali ambayo inapingana na maisha ya kiutu. Kwa hivyo kuumwa kwake si maradhi bali kuko akilini mwake. Hii ndio sababu daktari hawezi kutambua wala kutibu ugonjwa wake kwa kuwa unatokana na mifumo ya kibepari inayoendelezwa na daktari mwenyewe. Hii ndiyo sababu katika ndoto Sele anawaona madaktari wa kigeni wakiwa wanaukimbia na kuung’ang’ania moyo wake. Anaeleza kwamba:

SELE: Basi wale **madaktari** wakawa wananzungukazunguka... Waliposhindwa kupata chochote nikaona wamechukua vyembe vyao... Wazo likanija la kuwatapikia moyo wangu! ... Wote **wakaukimbia**... Nikajua hawakuja kuutibu mwili wangu bali kuutwaa moyo wangu...

ZAINABU: Mwanangu, labda hiyo ni ndoto tu (*Kijiba cha Moyo*, msisitizo wetu)

Ingawa kuna takriban miaka arobaini tangu mataifa ya Kiafrika yajipatie uhuru, magonjwa sugu huagiziwa madaktari kutoka mataifa yaliyoendelea jambo ambalo huendeleza utegemezi. Daktari

mkuu anayemshughulikia Sele ni wa kigeni. Jamila ni Mwafrika aliyesomea udaktari lakini anamtegemea daktari mkuu ili aweze kutoa uamuza kuhusu ugonjwa wa Sele.

SELE: Nilijua ... sina tatizo ... Hamkutaka kunisikiliza. Mnataka ... mtamke wenyewe ndo iwe sina tatizo. Ni njia rahisi kunitawala fikra na mwili. Na wewe hupendi nikuulize zaidi nikudadisi upembuzi wangu kunihusu. Daktari ni hata zaidi. Mnazichuma habari kunihusu kutoka kwangu halafu mnazijengea mnara kunitenga nazo ... Mnaiondoa stara yangu huku mafahamu heshima ya mtu ni stara yake. Uchi humuumbua mtu akabaki mithili ya gofu bovu. Kivuli chake tu. Na nyinyi mnajua (*Kijiba cha Moyo*: 62).

Kwa hivyo waandishi hawa wametumia ugonjwa na matibabu kuonyesha jinsi wageni walivyo-kuwa wakihuksika na kuwanyanya wenyeji huku wakijificha chini ya mwavuli wa kutoa usaidizi wa huduma ya matibabu. Aidha wanaonyesha kuwa madaktari wa kigeni walikuja kuendeleza ubepari wa mataifa yao. Huu ndio ukweli unaofikiwa na Sele katika *Kijiba cha Moyo* na Kitaru katika *Mashetani*. Wote wanatoa kauli kuwa waliyokuwa wakiyaona ndotoni yalikuwa ukweli. Wanaeleza:

KITARU: [...] Nikaanza kunyonyoa manyoya yangu. Lakini kila nikijinyonyoa, mengine yanaota [...] makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko yale. [...] Wazee wangu wakamwita daktari. Naye daktari ana manyoya kama sisi, ke mengi zaidi. [...] Imechukua muda mrefu **kutambua kuwa niliyo nikiyaona siyo ndoto au fikira mbovu, bali ni ukweli** wa kawaida. (*Mashetani*: 48-49, msisitizo wetu).

SELE: **Hata ndoto ni nusu ya kweli.** Huwezi kuota kisichokuwepo. Lakini mimi najua huu ni ukweli nilioushuhudia mwenyewe. (*Kijiba cha Moyo*: 81, msisitizo wetu)

Katika tamthilia hizi mbili, kuna wale wanaeleza ugonjwa wa wahusika hawa wakuu waki-zingatia itikadi za Waafrika kuhusu magonjwa yasioleweka. Kulingana na itikadi hizo, magonjwa yasioleweka huhushishwa ama na pepo au shetani kama ishara ya ushirikina wa Kiafrika. Watunzi wa tamthilia hizi wanaurejelea muktadha ulio sawa unaoelezea imani ya jamii za kale. Kwa mfano kuna vifungu vinavyorejelea itikadi hizi katika tamthilia zote mbili. Mathalan:

MAMA: Namwogopea Kitaru. **Mimi nafikiri kakumbwa na shetani** maana hawa wanakwenda **kucheza mbuyuni**, ule mbuyu mkubwa. Na mimi, ninajua ule mbuyu una mbaya. Una hatari kweli kweli. (*Mashetani*: 27, msisitizo wetu).

SELE: Siyo mashetani. Pepo hasa! **Mashetani hupatikana mibuyuni.** Na **kila mbuyu una shetani wake** lakini pepo hawadhibitiwi... (*Kijiba cha Moyo*: 4, msisitizo wetu)

BI RAHMA: (Anatazama.) Hivi nini? Siku ile nilipokuja kumwona hakuwa hivi. **Labda amepagawa na pepo!** (*Kijiba cha Moyo*: 40, msisitizo wetu)

Kutokana na vifungu hivi, inabainika kuwa jamii ya Mashetani inaamini kuwa mashetani huwa na makao yao kwenye miti mikubwa kama vile mibuyu na kwamba yejote anayechenza kwenye makazi ya mashetani basi hana budi kupagawa na mashetani wale. Imani sawa na hii inadhihirika

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

katika jamii ya Kijiba cha Moyo wakati tunapoambiwa na Sele kuwa mashetani hupatikana mibuyuni. Aidha imani kwamba mashetani hukaa mibuyuni inafafanuliwa zaidi na kauli inayosisitiza kuwa kila mbuyu una shetani wake. Kwa hivyo inabainika kuwa imani hii imezilemea jamii zinazolengwa na waandishi wa tamthila hizi mbili.

Mwingilianomatini Kijazanda

Uchunguzi wetu umebaini kuwa Hussein (1971) na Arege (2009) wametumia kunga zinazo-fungamanisha kazi zao na mazingira ya Kiafrika. Tamathali walizozitumia ni kama vile: hadithi, taswira, visakale, nyimbo na jazanda ili kufanikisha ujumbe wao. Kwa sababu ya lengo la makala haya ni kuonesha jinsi tamthilia hizi zinafanana kimatini, mjadala wetu umejikita tu kwenye matumizi ya jazanda. Jazanda ni mbinu inayoelezea jambo fulani kwa kutumia lugha ya kimafumbo au lugha fiche. Inapotumiwa, kile kinachorejelewa huwasilishwa kwa lugha isiyokuwa ya uwazi (King'ei 1987, Njogu & Chimerah 1999, Wamitila 2008). Kwa hivyo ujumbe unaowsilishwa huwa katika maneno yaliyotumiwa kuashiria jambo jingine.

Jazanda ya Abiria na Wenyewe Kushikwa na Dau

Katika tamthilia ya Mashetani, abiria ni taashira ya raia wa mataifa machanga ya Kiafrika. Raia hawa hushurutishwa kwenda kule wanakoelekezwa na nguvu za kibepari (mkondo). Kwa hivyo hawana uhuru wa kujiamulia ni upande upi wauelekee. Kadhalika ingawa kila taifa lina kiongozi wake, viongozi hao hawana uhuru wa kuendesha mataifa yao jinsi wanavyotaka. Badala yake wanaagizwa lipi wafanye. Hivi ndivyo Kitaru anavyomaanisha akisema:

KITARU: [...] toka tumepata uhuru, sisi Waafrika hapa imekuwa tumeingia ... ehe, mfano mzuri ... imekuwa kama tumeingia ... katika **jahazi** moja zuri na jina letu limeandikwa. Lakini ... **nahodha** ... nahodha nani? [...] je **mkondo** ukiwa unavutia upande mwengine, na nahodha anataka kupeleka **jahazi** upande mwengine? (*Mashetani*: 21, msisitizo wetu)

Kwa upande mwengine, Arege ametumia jazanda ya wenye kushikwa na dau akiashiria raia wa taifa fulani lililohuru. Kadhalika anatumia jazanda ya wenye kulishika dau kumaanisha viongozi wa taifa hilo. Mtunzi huyu anaonyesha kuwa kila mara raia na viongozi wake huchukuliwa kama washika dau hadi pale wanapoelezwa na mtu mwengine (mkoloni mamboleo) kuwa kuna wenye kulimiliki lile dau na wanadhibiti maongozi ya dau lile. Vifungu vifuatavyo vinashadidia maelezo haya.

ZAINABU: Pamoja na hayo, sisi vilevile ni **washika dau**. Ingefaa kutushirikisha mapema.

MUSA: Wajua katika **dau**, kuna **wenye kulishika na wenye kushikwa na dau**. Na wakati mwengine **dau** tofauti si dhahiri. Kwa ujumla huchukuliwa kuwa wote wanaoliabiria ni washika dau mpaka pale anapotokea mtu nakueleza kuwa **wenye dau** wapo na wamelitia mkononi. (*Kijiba cha Moyo*: 24-25, msisitizo wetu)

Katika bahari kuu (mfumo wa kiuchumi ulimwenguni), mataifa haya hutatizwa na nguvu za kibepari ambazo hutishia kuyaangamiza. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mashetani*, jahazi hudhibitiwa na nguvu za mkondo ambazo huamua ni upande upi jahazi lile lipelekwe. Nguvu za mkondo huu hutatiza lengo la nahodha ambaye mwishowe huishia kulipeleka jahazi lile upande yeze pamoja na abiria wake hawataki. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* dau na vilivyomo (abiria na viongozi) hudhibitiwa na nguvu za wenye dau na ambao ndio huamua ni upande upi dau lile lielekezwe.

Kutokana na jazanda hizi, inabainika kuwa kuna mtagusano kati ya raia na viongozi wa mataifa ya Kiafrika kwa upande mmoja na mataifa ya kibepari kwa upande mwingine. Katika mahusiano ya namna hii, mataifa ya kibepari (madola makuu) hudhibiti sera za kiuchumi na siasa za mataifa machanga. Uhusiano huu umefafanuliwa na watanzi wa tamthilia hizi kuwa ni wa mwenye nguvu mpishe. Jazanda za dau, wenye dau, walioshika dau, na walioshikwa na dau zilizotumiwa na Arege katika *Kijiba cha Moyo* ili kukuza na kufafanua maudhui ya ukoloni mamboleo ni mwangwi wa jazanda za jahazi, mkondo, nahodha na abiria zilizotumiwa na Hussein katika tamthilia tangulizi ya *Mashetani*. Kwa hivyo ni kauli ya utafiti huu kwamba Arege amefafanua dhana zilizotumiwa na Hussein katika *Mashetani*. Kwa hivyo kuna udugu wa kimatini baina ya tamthilia ya *Mashetani* na ya *Kijiba cha Moyo* hivi kwamba ukisoma mfano wa dau, wenye dau, washika dau, na washikwao na dau katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, una-kumbushwa ule mfano wa jahazi, nahodha, mkondo na abiria katika *Mashetani*.

Jazanda ya Bahari Kuu na Mkondo

Bahari ni eneo kubwa la maji linalozingira mabara na visiwa na huwa makazi ya viumbe kama vile papa, vidagaa, mkizi, nyangumi na wengineo. Aidha kuna itikadi kuwa kuna pepo waovu watokao mle baharini na walio na uwezo wa kuangamiza watu wakiwa katika kilele cha starehe zao (*Kijiba cha Moyo*: 4). Katika makala haya, ‘bahari kuu’ ni kielelezo cha mfumo wa kiuchumi ulimwenguni. Mwandishi wa *Mashetani* ametumia dhana ya bahari kuashiria ulimwengu unaomilikiwa na nguvu za kibepari. Kwa mfano, Kitaru anaeleza kuwa:

“Hadithi ya chewa. Mbali sana, ukivuka **bahari** saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na **mkondo** wa maji, ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali ni shetani.” (*Mashetani*: 28, msisitizo wetu)

Eneo hili kubwa la maji hukusanya pamoja samaki wa aina nyingi kama vile chewa, papa, vidagaa, mkizi, nyangumi na wengineo. Watunzi wa tamthilia hizi mbili wametumia maisha ya baharini kumulika maisha halisi katika ulimwengu wa kiuchumi unaomilikiwa na mabepari. Viumbe wakubwa wanaoishi baharini kama vile chewa na papa ni viashiria vyatya madola makuu ulimwenguni. Jinsi samaki hao wanavyodhihirisha nguvu na uwezo wao mle baharini, ndivyo

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

madola makuu ulimwenguni huwafanya mataifa machanga katika maisha ya kiuchumi na kisiasa katika ulimwengu halisi wa binadamu. Jinsi samaki hao wanavyowahangaisha vidagaa mle baharini ndivyo mataifa makuu huyahangaisha mataifa machanga.

Mkondo ni njia ya maji katika bahari inayopitisha maji kwa kasi na kwa nguvu. Katika utafiti tahakiki yetu, mkondo ni taashira ya nguvu za kibepari zinazomiliki uchumi na siasa za ulimwengu mzima. Kwa mfano, katika tamthilia ya Mashetani, jahazi hudhibitiwa na nguvu za mkondo ambazo huamua ni upande upi jahazi lile lipolekwe. Nguvu za mkondo huu hutatiza lengo la nahodha ambaye mwishowe huishia kulipeleka jahazi lile upande asiotaka ambapo ye ye wala abiria.

KITARU: [...] toka tumepata uhuru, sisi Waafrika hapa imekuwa tumeingia ... ehe, mfano mzuri ... imekuwakama tumeingia ... katika jahazi moja zuri na jina letu limeandikwa. Lakini ... nahodha ... nahodha nani? [...] je **mkondo ukiwa unavutia upande mwingine, na nahodha anataka kupeleka jahazi upande mwingine?** (*Mashetani*: 21, msisitizo wetu)

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, dau na vilivyomo (abiria na viongozi) hudhibitiwa na nguvu za wenye dau na ambao ndio huamua ni upande upi dau lile lielekezwe. Wenye dau ni kauli inayonuia kuonyesha umiliki wa kitu fulani. Kauli hii inarejelea ile dhana ya mkondo iliyotumiwa katika tamthilia tangulizi ya *Mashetani*. Kwa hivyo wenye dau ni madola makuu yanayomiliki nyezo za uzalishaji na ugavi wa mali katika ulimwengu unaomilikiwa na nguvu za kibepari. Hili linashadidiwa na kifungu kifuatacho:

MUSA: Wajua katika dau, kuna wenye kulishika na wenye kushikwa na dau. Na wakati mwingine dau tofauti si dhahiri. Kwa ujumla huchukuliwa kuwa wote wanaoliabiria ni washika dau mpaka pale anapotokea mtu na kueleza kuwa **wenye dau wapo na wamelitia mkononi**. (*Kijiba cha Moyo*: 24-25, msisitizo wetu)

Jazanda hizi zimetumiwa kukuza na kufafanua uhusiano wa kinyama uliopo baina ya mataifa makuu na mataifa machanga. Uhusiano huu haujajengwa kwenye misingi ya usawa na utu. Kadhalika bahari imetumiwa kuendeleza mivutano inayofafanua maudhui ya ukoloni mamboleo, utegemezi, dhuluma na unyanyasaji pamoja na ukosefu wa uhuru kamili.

Mwandishi wa *Kijiba cha Moyo* ametumia bahari kuashiria ulimwengu unaomilikiwa na mfumo wa kiuchumi wa kibepari. Anaonyesha kuwa kuna nyakati bahari huwa na raha zake. Pia anabainisha kuwa bahari ina hatari zake ambazo zinastahili kutorokwa na waja. Kwa hivyo, mtunzi huyu ametumia maisha ya baharini kumulika jinsi maisha yalivyo katika ulimwengu wa kiuchumi unaomilikiwa na mabepari. Kwa mfano Sele anaeleza:

SELE: ... **Raha hasa! Kama vile ilivyotokea baharini**. Wanakutwaa katika kilele cha starehe. Ushaona? (*Kijiba cha Moyo*: 4, msisitizo wetu)

SELE: ... Unafikiri kwa nini mandhari yawe yanapendeza ufuoni? Kwa nini wakati huu huo upepo mwanana uvume na **siyo kwenda baharini?** Eee! **Vipi bahari itoe pasi kupokea?** Tena siku zote! Huoni kuna jambo? (Kwa msisitizo.) **Pepo hutoka baharini** na hawatulii ... (*Kijiba cha Moyo*: 5, msisitizo wetu)

Jazanda hii imetumiwa kukuza na kufafanua uhusiano uliopo baina ya mataifa makuu na mataifa machanga ambao ni wa mwenye nguvu mpishe.

Jazanda ya Ugonjwa wa Kitaru na Sele

Katika tamthilia ya *Mashetani*, ugonjwa wa Kitaru unaelezwa na wale anaoingiliana nao kuwa ni ugonjwa wa mashetani, mizuka, wasiwasi, machofu ya akili au kuendekeza akili. Ugonjwa huu ni jazanda inayoashiria mgongano wa nafsi zake mbili zinazokinzana. Hali hii inamwingiza kwenye mtafaruku mkubwa wa kiakili na kumfanya awe na fikira zinazogongana na kuzozana. Kwa hivyo ugonjwa wa Kitaru ni fikira alizonazo kuhusu vile anavyoweza kutoka katika hali hii ya ukabaila na kisha aweze kujenga uhusiano ulio na maana.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* Sele amesawiriwa akiwa anaumwa. Ugonjwa wake ni jazanda inayofafanua mgongano wa nafsi zake mbili zinazokinzana. Anajua kwamba kuna kasoro fulani katika jamii anamoishi iliyosababishwa na kuweko kwa nguvu za kikoloni. Nguvu hizo huamua mkondo wa kisiasa na kiuchumi katika taifa lao lililo ‘huru’. Isitoshe, anaelewa kuwa mataifa ya kibepari huyaonea na kuyanyanyasa mataifa machanga kwa kuingilia njia za uzalishaji na ugavi wa mali ya mataifa yao. Ugonjwa wake unaashiria matatizo yanayokumba mataifa machanga ya Kiafrika. Matatizo hayo husababishwa na athari za ukoloni mamboleo.

Motifu ya Safari

Motifu ni kipashio kinachotumiwa kukuzia au kuiweka wazi dhamira ya mtunzi. Aidha motifu ni kipengele kidogo cha mtindo kisichoweza kugawika zaidi. Mwingilianomatini unaweza kujitokeza katika kiwango cha motifu. Motifu ya safari ni harakati za binadamu kujisaka ili kujitambua kimawazo (Wamitila 2002).

Baada ya kipindi fulani cha kufurahia uhuru, viongozi na wananchi wa Tanzania walianza kukumbwa na matatizo kuhusu uhalisia wa ‘uhuru’ walioupewa. Mwanzoni walimlaumu mkoloni kama mwenye kuyasababisha. Baadaye walitambua kuwa kumlaumu hakungewafikisha mbali na hivyo basi waliamua kuitisha Azimio la Arusha (1967) liwe mwongozo wao wa kisiasa, kiuchumi na kijamii katika harakati za ujenzi wa jamii ya kijamaa (Njogu & Chimerah 1999). Binadamu anaeleza kuwa:

“Kosa limefanyika. Sasa lililobaki ni azimio; kosa hili halifanyiki tena, wala halitafanyika tena [...] nina haja na vitu vitatu - bidii, ari na ukweli [...] Kuna lile lipasalo kufanywa, na yule apasaye kulifanya. Kuna kitendo na mtendaji [...] Mtendaji ni mimi.” (*Mashetani*: 11-12)

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Kulingana na dondo hili, Binadamu (anayewakilisha raia na viongozi) alipotambua kuwa kosa lilifanyika anaazimia kutafuta ukweli. Azimio hili linakuwa mwanzo wa safari ndefu ya kujitafuta, kujisaka ili ajijue yeye ni nani pamoja na kujua historia ya jamii yake. Anataka ajijue yeye ni nani wa kutekeleza azimio lile. Anatujuvya:

“Mimi ni nani? Mimi-mimi au yeye-mimi anayetaka kuitekeleza azimio hili?”
(*Mashetani*: 12)

Kujitambua huku ni kuelewa historia ya taifa lao pamoja na maana ya uhuru walioupewa na mkoloni. Kujitambua huku kungewawezesha kuelewa vyema azimio lilokuwa mbele yao. Hii ndiyo sababu Binadamu (anayewakilisha raia) kujisaka na kujija kwake kunampitisha kwenye safari ndefu. Anasema:

“Lazima nisafiri, safari ndefu, nikajitafute, nikajisake ili nijijue mimi nani? Ili nijue maana ya kitendo changu.” (*Mashetani*: 12)

Viongozi wa Kiafrika walielewa wazi kuwa Azimio lile, uhuru wao pamoja na maisha ya raia wao hayangekuwa na maana bila ya viongozi na raia kujija wao ni kina nani (Njogu na Chimerah 1999). Kujija huku kulikuwa ni kuifahamu historia ya taifa lao, maana ya uhuru wao na pia umuhimu wa Azimio lao la ujenzi wa taifa mpya la kijamaa. Ukweli kuhusu historia na hali ya taifa lao katika siku za mbeleni ungepatikana kutokana na kujija huku. Binadamu anasema:

“Mimi ni nani? Mimi-mimi au yeye- mimi anayetaka kulitekeleza azimio hili? Kama sijui ukweli wa [...] kitendo changu, maisha yangu wala azimio langu lazima nisafiri, safari ndefu, nikajitafute, nikajisake ili nijijue mimi nani? Ili nijue maana ya kitendo changu.” (*Mashetani*: 12).

Wafula (1999) anaeleza kuwa baada ya msimamo huu kuchukua, uhusika wa Binadamu anabadilika na kuwa Kitaru, mwanachama wa jamii ambayo imechukua nafasi ya mkoloni anapo-toweka. Msako unapoanza, Kitaru anaanza kujifungia chumbani mwake akipekua historia ya jamii lake. Anasoma kitabu kiitwacho *Outline of African History* ili aielewe vyema historia ya jamii yake kabla ya majilio ya wakoloni. Kadhalika anataka kufahamu asili ya ubwanyenye wa familia ya kina Juma, na jinsi mapinduzi ya kijamaa ya 1964 yalivyobadilisha maisha ya jamii nzima ya taifa la Tanzania. Ufahamu huu ungemsaidia kutafuta uhusiano ulio na maana baina ya tabaka lake na la Juma. Anakiri kwamba tangu aanze kusoma vitabu vya historia ameanza kuathirika kimawazo (Njogu na Chimerah 1999). Kitaru anasema:

“Sielewi namna gani au kwa nini nimesomea law katika University. Toka kuanza kusoma soma hivi vitabu vya Historia mawazo yangu yamebadilika bwana. Ingwezekana, ningebadilisha *faculty*. Haki tena.” (*Mashetani*: 16)

Kitaru anagundua kuwa hali ya kinaizi ya familia yao ilitokana na mapinduzi ya kijamaa ya 1964. Baada ya mapinduzi haya, milki ya mabwanyenye ilichukuliwa na kupewa watu wa tabaka la

chini ikiwemo familia yao. Anatambua kuwa umaskini wa akina Juma unatokana na mali yao kuchukuliwa na kupewa maskini kama wao (uk. 38). Vilevile anagundua kuwa manaizi kama Babake wanajigamba kwa mali na ubinafsi wao. Kwao, vitu kama gari, pesa, mke, anasa na mapato ndivyo vya thamani. Mambo haya yanafanya Kitaru atambue kuwa jamii yake inasumbuliwa na tamaa ya kutaka kujilimbikizia mali bila kuwajali raia.

Safari hii ya kujisaka inaonyesha kuwa hali ya sasa ya familia ya kina Juma imesababishwa na kuweko kwa ukoloni mamboleo. Katika msako wa mahusiano baina ya jamii yake na wakoloni, Kitaru anautumia mfano wa jahazi ili kufahamu vizuri uhusiano uliopo. Anatambua kuwa mataifa ya Kiafrika yamefungamanishwa kiuchumi na kisiasa na mataifa ya wakoloni na wakoloni mamboleo. Kwa sababu hii viongozi hawawezi kulipeleka jahazi wanakotaka, bali jahazi hili huvutwa na mkondo (nguvu za kikoloni) na kuelekezwa kule mkondo unakotaka (King'ei 1987). Uhusiano huu baina ya mataifa ya Kiafrika na mataifa makuu ni mojawapo ya hali ambazo Kitaru anazozisaka azijue na kuzielewa.

Katika harakati za kujisaka, Kitaru anatambua kuwa hawezi kupata msaada wowote kutoka kwa wazazi wake (tabaka la kinaizi) kwa sababu hawalielewi tatizo lake. Kwa mfano, anapozungumzia ‘shetani’ (mtu aliye mwovu) wanafikiri ni ‘shetani’ pepo tu. Anapokosa usaidizi kwa wazazi, anaamua kuutafuta kwa Mfaume (tabaka la chini) (King'ei 1987). Mfaume anamhakikishia Kitaru kwamba mashetani (nguvu za ukoloni mkongwe) wapo ni vile tu raia wamezibwa macho wasiwaone. Mfaume anasema:

“[...] Juzi juzi hapa, dereva mmoja bwana [...] Mara peke yake bwana kachepuka njia akenda kulilaza basi miguu juu chini. Kaulizwa. Kwani kasema nini? Kasema, ‘Shetani kazi ya shetani,’ Kaona njia mbili. [...] Mashetani wapo. [...] lakini tumezibwa macho tu, hatuwaoni.” (uk. 29)

Hata hivyo nguvu za ukoloni mkongwe (mashetani) huwasumbua Waafrika. Aidha Kitaru anafahamikiwa kwamba hali hii ya ‘ushetani’ (unaizi) ndiyo inayomtenganisha na Juma.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, raia wa mataifa ya Afrika walitambua kuwa mwongozo wa kisiasa na kiuchumi katika mataifa yao ulikuwa ukitolewa na mataifa ya kigeni na wala si viongozi waliowachangua. Mtunzi wa *Kijiba cha Moyo* anawarai viongozi na raia wa mataifa ya Kiafrika wajisaili ili wajue wao ni kina nani katika ulimwengu unaomilikiwa na mfumo wa kibepari. Kujijua na kujisaili ni kuifahamu historia ya mataifa yao, maana ya uhuru wao na pia umuhimu wa ujenzi wa jamii mpya yenye usawa na uhusiano wa kiutu. Aidha, anaonyesha kuwa suluhu ya matatizo yao imo katika kujua ukweli wa kihistoria jamii yao siku za mbeleni. Hii sababu raia (Sele) wanaamua kujisaka na kujisaili wajue wao ni kina nani katika mahusiano baina yao na mataifa yaliyoendelea. Sele anasema:

“ ... Ninajaribu kutafakari kwa makini uhusiano baina yao na sisi. Na vilevile kudadisi sisi ni kina nani katika uhusiano huo. (Kimya.) (*Kijiba cha Moyo*: 29)

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

Sele anapoamua kujisaka na kujisaili anaanza kujifungia chumbani mwake akitafakari na kuchunguza uhusiano baina ya jamii yake (mataifa ya Kiafrika) na mataifa wafadhili (Wakoloni-maboleo) na pia baina ya Waafrika wenyewe kwa wenyewe. Msako huu unaiumiza nafsi na akili yake. Kuumwa kwake kunasabishwa na msukumo wa kutaka afahamu vyema uhusiano wa kijamaa katika jamii yake kabla ya majilio ya wakoloni, pamoja na athari za baada ukoloni. Vilevile anataka kufahamu asili ya ubepari wa madola makuu, na jinsi mfumo wa kibepari ulivyobadilisha maisha ya kijamaa ya Waafrika. Ufahamu huu utamwezesha kuwa katika nafasi bora ya kutafuta uhusiano wenyewe maana kati ya jamii yake Kiafrika na wafadhili. Sele anakiri kwamba alipoanza kuchunguza upya historia iliyosababisha uhusiano usiokuwa na usawa ameathirika kihisia na kimawazo. Anasema:

“Ndio huu ukurasa mpya niliofungua. Kuuangalia upya udugu wetu. Na baada ya kuuangalia kwa makini ninaanza kujichukia. ... ni kama sisi si kitu mbele yao. ... Na muda huu wote ni kama sisi hatukutambua. Tunapakwa mafuta kwa mgongo wa chupa, nasi twaridhia tu.” (*Kijiba cha Moyo*: 29)

Msako wake unafafanua kuwa uroho wa wakoloni wakongwe umerithiwa na wakoloni mamboleo. Aidha, anaonyesha kuwa wivu, kiburi, pupa na tamaa ya wakoloni wakongwe inayoendelezwa na wakoloni mamboleo. Ulaghai na udanganyifu uliotumiwa na wakoloni wakongwe kujipenyeza na kukalia baadhi ya sehemu za Afrika wakidai kuwa walikuja kuwafaidi Waafrika, ndio wanaoutumia wakoloni mamboleo kujipenyeza kwa mataifa ya Kiafrika kupitia utoaji wa ufadhili kama ndugu weza. Daktari anaeleza:

Mimi niko hapa kukufaa. Ukitaka nirudi nitarudi. Maarifa nimekuja nayo. Ala za kazi nimekuja nazo vilevile kutoka huko mbali. (*Kijiba cha Moyo*: 54)

Dondoo hili linafafanua kuwa ufadhili wa mataifa makuu hulenga tu kunyanyasa mataifa ya Kiafrika. Maarifa na ala za kutekeleza miradi inayofadhiliwa hutoka kwa wafadhili hao. Kwa hivyo asilimia kubwa ya ufadhili huo huwafaidi walioutoa. Kwa jinsi hiyo mataifa wafadhili huendeleza ubepari wao chini ya mwavuli wa kuyasaidia mataifa ya Kiafrika. Utambuzi huu unamfanya Sele afichue unafiki wao kwa kumwambia Daktari:

Nilijua tangu hapo kuwa kipo kitu. Nilihis i kama utanichezea ila sikutaka kukushuku kabla kushuhudia. Sasa nimeshuhudia... Siku nyingi umenichezea lakini ukawa unakuficha huko kunichezea kwako. Sasa najua hukuja kwa kunijali. Umekuja kwa manufaa yako uliyoyaficha katika hoja yangu. (*Kijiba cha Moyo*: 56)

Kutokana na dondoo hili, inabainika kuwa historia inayorejelewa na Sele inamfanya aelewé jinsi wakoloni wakongwe walivyojinufaisha kwa kuyapakua malighafi na maliasili ya bara Afrika huku wakidai walikuja kuwanufaisha Waafrika. Baada ya kujinufaisha, waliwapa Waafrika uhuru wa bendera lakini wakabakia wakiendeleza ukoloni mamboleo. Utawala huu mpya ultiliwa mbolea na mfumo wa kibepari uliotoka nje ya bara Afrika. Vilevile, anagundua kuwa wafadhili husema wamekuja kutatua shida za Afrika walakini huwa wamekuja kuendeleza biashara za

AMBROSE K. NGESA, ENOCK MATUNDURA & JOHN KOBIA

kuwafaidi wao wenyewe. Sele anayachukulia matibabu ya daktari kuwa biashara. Anatoa maelezo yafuatayo:

Si biashara hiyo? Wautumie mwili wangu kujinufaisha! (uk. 77)

Zipo siku za nyuma niliposhawishika kuwaamini. Siku hizo nilitaka wanifae. Hawakunifaa. Walinichezea. Mwili wangu hawakuufanya chochote cha kuuthamini. Wao ndio walinifanya kuamini kuwa nina ugonjwa. Tena ugonjwa mbaya. Ugonjwa unaotaka msaada wao. Niliwaamini ... Walinifanya kuamini kuwa wao ndio suluhisho la matatizo waliyoniambia yananitatiza ... Mpaka leo bado wanataka niamini kuwa nina tatizo... Wameliumba katika ... fikra yangu na wao wanataka niamini kama kweli lipo na kwamba wao tu ndio wawezao kulisuluhisha. ... Wanataka niamini nilivyoamini jana. (Kimya.) Wote nawajua. (k. 77-78)

Kwa hivyo, Arege anashadidia kuwa wakoloni wakongwe na hata wakoloni mamboleo hawakuwafaa Waafrika kwa lolote bali walichokifanya ni kuwafanya waamini kuwa wana ugonjwa mbaya sana unaoweza tu kutibiwa na wakoloni wale. Mwanzoni Waafrika waliwaamini wageni hao, lakini hawakuweza kubadilisha hali yao duni. Walichokifanya wakoloni ni kuya-fungamanisha mataifa ya Kiafrika na mataifa makuu duniani kiuchumi na kisiasa kupitia kwa viongozi wao. Hata hivyo, mahusiano hayo hayakuwa na usawa bali ya mwenye nguvu mpishe.

Juhudi za kusaka uhusiano baina ya jamii yake na madola makuu zinamwezesha kutambua kuwa madola makuu huwa na kiburi kwa mataifa yanayostawi. Aidha aligundua kuwa madola makuu yakinaka kunyanyasa mataifa machanga huchochea michafuko ya kiuchumi na kisiasa ulimwenguni. Ukosefu wa uhuru wa kujiamulia masuala muhimu unamghadhabisha Sele na kumpa msukumo wa kutamka:

Hata si wao walioituachisha. Wanatuhitaji lakini wamepewa amri na ndugu zetu washirika kupitia mikopo yao. Si habari ya sisi kuchangua. Ni sisi tutii. Tutatii amri zao mpaka lini? (*Kijiba cha Moyo*: 29)

Kadhalika, Sele anatumia mfano wa dau kueleza ukoloni mpya unaoyakumba mataifa machanga ya Kiafrika. Jazanda ya ‘dau, washikwa na dau, washika dau na wenyewe kulidhibiti dau’ inadhi-hirisha jinsi mataifa ya Kiafrika yalivyo fungamanishwa na madola makuu duniani kupitia uchumi na siasa. Uhusiano huu unawafanya walishikao dau (viongozi) wakose kulipeleka kule watakako kwa kuwa limedhibitiwa na nguvu za waliolitia mkononi (wakoloni) ambazo hulielekeza kule zinakotaka. Uhusiano wa namna hii ni kijiba kinachomsumbu Sele na kumfanya aonekane mwenye kuumwa. Anajifungua chumbani mwake ili asaili na kuusaka uhusiano wa kidhuluma baina ya jamii yake na wafadhili na mwishowe kuutafutia uhusiano huu suluhu mwafaka. Sele anaeleza Bi Rahmah kuwa:

Sikiliza bibi, hivi ninavyokaa hapa nyumbani si kwamba nimekata tama. La hasha! Ninajaribu kutafakari kwa makini uhusiano baina yao na sisi. Na vilevile kudadisi sisi ni kina nani katika uhusiano huo. (Kimya.) (*Kijiba cha Moyo*: 28-29)

MWINGILIANOMATINI KATIKA *MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO*

Harakati za msako wa Sele zinamwingiza kwenye mjadala baina yake na Daktari aliyeitwa aje kumtibu yeye kutokana na fikra zake zisizofungamana na mfumo wa kibepari. Sele anatumia lugha ya kifalsafa kumwelezea Daktari mawazo na fikira zake nzito. Daktari anashindwa kui-elewa moja kwa moja dhana ya ‘kutopenda na kupenda’, ‘mbili ongeza mbili’ na pia ‘mbili mara mbili’ (k. 71-72) na vilevile dhana za ‘daktari’ na ‘uso-daktari’ na ‘refa’ na ‘uso-refa’. Sele anamwambia:

... Jisikilize kwanza kama huamini. (Kimya.) Hivi unavyonisikiliza, unanisikiliza wewe kama daktari au uso daktari ... Au acha nikuulize hivi, refa anapochezeshesha mchezo, mpaka kati ya yeye kama refa na uso-refa wake unaanzia na kuishia wapi? (*Kijiba cha Moyo*: 74).

Mwishowe Sele anagundua kuwa dhana hizo hulenga kitu kile kile kilichokuwa kikirejelewa mwanzoni na kwa hivyo ni pande mbili za sarafu ile ile moja. Utambuzi huu unadhihirisha kuwa daktari wa kikoloni na ukoloni wenyewe huendeleza shughuli ile ile moja ya ubepari. Vilevile hakuna tofauti kati ya refa na uso-refa wake kwa kuwa wote hushiriki kuuchezeshesha mchezo; mmoja (uso-refa) akiwa kikaragosi wa mwingine (refa). Kwa hivyo, dondoo hili inabainisha kuwa daktari wa kigeni anayekuja kumtibu Sele ni mwangwi wa nguvu za kibepari zinazomwongoza kutoka kwao kuja ‘kuwashudumia’ Waafrika.

Hitimisho

Katika makala haya, tumeonesha jinsi ambavyo tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* zinavyoingiliana kimatini. Tumetoa ushahidi kutoka kwa kazi hizi mbili kuonesha jinsi tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* iliyyotungwa takriban miongo minne baada ya *Mashetani* inavyochota, kuiga au kunukuu baadhi ya sehemu na vipengee vyta tamthilia hiyo ya *Mashetani*. Kwa hivyo, ni bayana kwamba kuna mwingilianomatini baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*. Kauli ambayo hatuwezi kuisema kwa uhakika ni iwapo kufanana huku kwa tamthilia hizi mbili kulisababishwa na kuathiriwa kwa mtunzi wa *Kijiba cha Moyo* na matini tangulizi ya *Mashetani* au ni mwigo wa kimakusudi ambao unasababisha tamthilia hizi kuwa kama shilingi kwa ya pili. Inaonekana kwamba Arege anapotumia kazi ya Hussein kimwingilianomatini kufanikisha utunzi wa tamthilia yake ya *Kijiba cha Moyo* (kwa kujua au kutojua) anachangia katika uchambuzi na uelewekaji wa tamthilia ya *Mashetani*. Hali hii hivyo basi inasababisha tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* kuwa na uchangamano unaoifanya isomeke kama *Mashetani* na kumfanya Arege awe ‘Ebrahim Hussein wa pili’ katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili. Katika kuibuka na tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Arege anaelekea kuvunja rekodi ya Hussein ya takriban miongo minne katika utunzi wa tammthilia ya Kiswahili kwa kutumia kiunzi cha mtangulizi wake kwa kuegemea umwingilianomatini.

Marejeleo

- Allen, Graham. 2000. *Intertextuality*. New York: Routledge.
- Arege, Timothy. 2007. *Chamchela*. Kenya, Jomo Kenyatta Foundation.
- Arege, Timothy. 2009. *Kijiba cha Moyo*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Arege, Timothy. 2009. *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Bakhtin, Mikhail M. 1981. *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin & London: University of Texas Press.
- Bakhtin, Mikhail M. 1986. *Speech Genres and Other Late Essays*. Austin & London: University of Texas Press.
- Barthes, R. 1979. From Work to Text. *Textual Strategies: Perspectives in Poststructuralism Criticism*, ed. by Josué Harari V.. Ithaca, NY: Cornell University Press. pp. 73-81.
- Bazerman, Charles. 2004. *Intertextuality: How Texts Rely on Other Texts*. Santa Barbara: University of California Press.
- Bazerman, Charles & Paul Prior. (eds) 2004. *What Writing Does and How It Does It. An Introduction to Analyzing Texts and Textual Practices*. Mahwah, NJ & London: LEA Publishers.
- Bertoncini-Zúbková, Elena. 1989. *Outline of Swahili Literature*. Leiden: E. J. Brill.
- Bloom, Harold. 1994. *The Western Canon*. New York: Harcourt Brace & Company.
- Bossinade, Johanna. 2000. *Poststrukturalistische Literaturtheorie*. Stuttgart & Weimar: J.B. Metzler.
- Bodunde, Charles A. 1994. Studies in Comparative Literature. *New Introduction to Literature*, ed. by Olu Obafemi, Mary Tinuoye & Charles Bodunde. Ibadan: Y. Books. pp. 55-74.
- Chacha, Nyaigotti C. 1986. *Marejeo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Clayton, Jay & Eric Rothstein. 1991. Figures in the Corpus: Theories of Influence and Intertextuality. *Influence and Intertextuality in Literary History*, ed. by Jay Clayton & Eric Rothstein. Madison & Wisconsin: The University of Wisconsin Press. pp. 3-36.
- Coyle, Martin, Garside Peter, Kelsall Malcolm & John Peck. 1990. *Encyclopedia of Literature and Criticism*. London: Macmillan.
- Culler, J. 1975. *Structuralist Poetics*. London: Routledge & Kegan Paul.

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

- Culler, J. 1983. *On Deconstruction: Theory and Criticism after Structuralism*. New York: Cornell.
- Diegner, Lutz. 2005. Intertextuality in the Swahili Contemporary Novel: E. Kezilahabi's Nagona and William E. Mkufya's Ziraili na Zirani. *Swahili Forum* 12: 25-35.
- Eangleton, T. 1983. *Literary Theory: Introduction*. Oxford: Blackwell.
- Enani, M. M. 1995. *Comparative Tone: Essays in Comparative Literature*. Cairo: GEBO.
- Fiebach, Joachim. 1997. Ebrahim Hussein Dramaturgy: A Swahili Multiculturalists Journey in Drama and Theatre: *Research in African Literatures* 28, 4: 19-37.
- Mugenda, Olive M. & A. G. Mugenda. 2003. *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: African Centre for Technology Studies.
- Genette, Gérard. 1988. Strucuralism and Literary Criticism. *Modern Criticism and Theory: A reader*, ed. by David Lodge & Nigel Wood. London & New York: Longman. pp. 62-78.
- Genette Gérard. 1997. *Palimpsests: Literature in the Second Degree*. Lincoln & London: University of Nebraska Press.
- Gikandi, Simon. 1992. *Reading Chinua Achebe*. Potsmouth: Heineman
- Grass, Günter. 1962. *The Tin Drum*. New York: Vintage.
- Hudson-Champeon, Connie. 2010. *Conversations within Conversations: Intertextuality in Racially Antagonistic online Discourse*. United States: Bibles International.
- Hussein, Ebrahim. 1967. *Alikiona*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, Ebrahim. 1967. *Wakati Ukuta*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, Ebrahim. 1969. *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press
- Hussein, Ebrahim. 1971. *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, Ebrahim. 1976. *Jogoo Kijijini*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, Ebrahim. 1976. *Ngao ya Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hyslop, Graham. 1957. *Afadhal Mchawi*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Hyslop, Graham. 1957. *Mgeni Karibu*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Kehinde, Ayo. 2003. Intertextuality and the African Novel. *Nordic Journal of African Studies* 12, 3: 372–386.
- Kezilahabi, Euphrase. 1990. *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

AMBROSE K. NGESA, ENOCK MATUNDURA & JOHN KOBIA

- Kezilahabi, Euphrase. 1990. *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- King'ei, Kitula G. 1987. *Mwongozo wa Mashetani*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Kristeva, Julia. 1980. *Desire in Language: A Semiotic approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.
- Kristeva, Julia. 1984. *Revolution in Poetic Language*. New York: Columbia University Press.
- Kristeva, Julia. 1986. The Kristeva Reader, edited by T. Moi. Oxford: Basil Blackwell.
- Lemke, J. L. 1985. Ideology, Intertextuality, and the Notion of Register. *Systemic Perspectives on Discourse*, ed. by J. D. Benson & W. S. Greaves. Norwood N. J: Ablex. pp. 275-294.
- Maidi, Naïma. 2008. *Literary Affinities and Influences*. M.A Dissertation. University M'hamed Bougara, Algeria.
- Matundura, Enock. 2011. What ails Kiswahili Literature. *Sunday Nation: Life & Style*. Nairobi: Nation Media Group.
- Matundura, Enock. 2012. *Mashetani ni Tamthilia ya Upeo wa Juu*. *Taifa Leo*. Nairobi: Nation Media Group.
- Mazrui, A. 1982. *Kilio cha haki*. Nairobi: Longman.
- Mishra, Raj K. 2012. A study of Intertextuality: The Way of Reading and Writing. *Prime Research on Education* 2, 3: 208-212.
- Mukobwa, M. 1985. *Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia Tano za Hussein*. Tasnifu ya M.A. Nairobi: University of Nairobi.
- Mulokozi, M. M. 1988. *Mukwawa wa Uhehe*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Muriithi, J. 2002. *Usemezano katika tamthilia ya Kiswahili: Mfano wa Mashetani, Kilio cha Haki na Amezidi*. Tasnifu ya MA. Nairobi: Kenyatta University.
- Mushi, S.S. 1968. *Makbeth*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mushi, S.S. 1968. *Tufani*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mutegi, M. J. N. 1985. *Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia za Ebrahim Hussein*. Tasnifu ya M.A. Nairobi: University of Nairobi.
- Njogu, Kimani. 1997. *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Njogu, Kimani & Rocha M. Chimerah. 1999. *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

MWINGILIANOMATINI KATIKA MASHETANI NA KIJIBA CHA MOYO

- Njogu, Kimani & Richard M. Wafula. 2007. *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njoroge, H. 2007. Mwingilianomatini katika Fasihi ya Kiswahili: Tata za Asumini na Rosa Mistika. Tasnifu ya MA. Nairobi: University of Nairobi.
- Northrop, F. 1990. *Anatomy of Criticism*. London: Penguin.
- Ntarangwi, Mwenda. 2004. Uhakiki wa kazi za fasihi. Phd Dissertation. Rock Island: Augustana College.
- Nwagbara, U. 2011. Intertextuality and The Truth of Achebe's Fiction: Militarised Nigerian Postcolonial in *Anthills of the Savannah*. *The African Symposium* 11, 2: 85-98.
- Nyerere, Julius. 1969. *Julius Kaisari*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Nyerere, Julius. 1969. *Mabepari ya Venisi*. Dar es Salaam & Nairobi: Oxford University Press.
- Plottel, Jeanine P. & H. Kurz Charney. 1978. *Introduction to Intertextuality: New Perspective in Criticism*. New York: Literary Forum.
- Ricard, Alain. 2000. *Ebrahim Hussein. Swahili Theatre and Individualism*. Nairobi: Mkuki wa Nyota Publishers.
- Rohde, Larissa. 2005. *The Network of Intertextual Relations in Naipaul's Half a life and Magic seeds*. PhD dissertation. Porto Alegre: Universidade Federal do Rio Grande do Sul.
- Said, A. 2000. Review of *Ebrahim Hussein: Swahili Theatre and Individualism* by Alain Ricard. *Nordic Journal of African Studies* 14, 3: 409-418.
- Syambo B. & A. Mazrui A. 1992. *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Wafula, Richard M. 1999. *Uhakiki wa Tamthilia Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, Richard M. 2003. Language and Politics in East African Swahili Prose: Intertextuality in Kezilahabi's Dunia Uwanja wa Fujo ("The World, a Playground of Chaos"). *Politics and Economics of Africa*, 4: 89-99.
- Walibora, Ken. 1996. *Siku njema*. Kenya: Longhorn.
- Wamitila, Kyalo W. 2002. *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, Kyalo W. 2003. *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus.

AMBROSE K. NGESA, ENOCK MATUNDURA & JOHN KOBIA

Wamitila, Kyalo W. 2008. *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanguzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Worton, Michael & Still, Judith. (eds). 1990. *Intertextuality Theories and Practice*. Manchester: Manchester University Press.